# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS, IKULU

*Dar es Salaam*
*05 Agosti, 2026*

Baruapepe: press@ikulu.go.tz

## TAARIFA KWA UMMA

### ZIARA RASMI YA RAIS YOWERI MUSEVENI WA UGANDA, NCHINI

Rais wa Jamhuri ya Uganda, Mheshimiwa Yoweri Kaguta Museveni, anatarajiwa kuwasili nchini leo, tarehe 05 Agosti, 2026, kwa ajili ya ziara, kwa mwaliko wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Akiwa nchini, Rais Museveni na mwenyeji wake, Rais Dkt. Samia, watafanya mazungumzo kuhusu kuimarisha uhusiano na ushirikiano kati ya Tanzania na Uganda, yakijikita katika biashara, uwekezaji, nishati, miundombinu, usafirishaji, ulinzi na usalama pamoja na masuala ya kikanda.

Ziara ya Rais Museveni inatarajiwa kuimarisha uhusiano wa kihistoria na kindugu kati ya Tanzania na Uganda, pamoja na kufungua fursa mpya za ushirikiano kwa manufaa ya wananchi wa nchi zote mbili.

Bakari S. Machumu
Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu